

## Learning by Ear 2011 – Road Safety

### Episode 03 – Pedestrian precautions

**Text:** Victoria Averill

**Editing:** Johannes Beck, Katrin Ogunsade

**Proofreading:** Martin Vogl

#### **CHARACTERS:**

Onyesho la 1:

- ▲ ALICE (MSICHANA, UMRI WA MIAKA 13) (+ chupa mbili)
- ▲ NANCY (MSICHANA, UMRI WA MIAKA 11, RAFIKIYE ALICE)

Onyesho la 2:

- ▲ NANCY (MSICHANA, UMRI WA MIAKA 11)
- ▲ ALICE (MSICHANA, UMRI WA MIAKA 13)

Onyesho la 3:

- ▲ NANCY (MSICHANA, UMRI WA MIAKA 11)
- ▲ ALICE (MSICHANA, UMRI WA MIAKA 13)

Onyesho la 4:

- ▲ ALICE (MSICHANA, UMRI WA MIAKA 13)
- ▲ MWENDESHA BAISKELI (MWANAMUME AU MWANAMKE)
- ▲ DEREVA (MWANAMUME AU MWANAMKE)

Intro/Studio/Outro:

- ▲ MTANGAZAJI BEATRICE (MWANAMKE)
- ▲ GEORGE – MTAALAMU WA USALAMA BARABARANI (MWANAMUME) □

Tah: Mtangazaji anaweza kuwa mwanamume na mtaalamu wa usalama barabarani anaweza kuwa mwanamke.

**Intro:**

**1. Beatrice:** Karibu kwenye makala ya Noa Bongo Jenga Maisha yako na pia michezo yetu ya redio kuhusu usalama barabarani. Ninaitwa Beatrice na nitakuwa nawe kwa muda wa dakika kumi zijazo. Kwenye vipindi kumi vitakavyofuata tutaandama na familia ya Wanjiru. Tutaangazia maisha yao ambapo walishuhudia maafa yanayotokana na ukosefu wa usalama barabarani barani Afrika. Tunazungumza pia na mtaalamu wa usalama barabarani ili tujue jinsi ya kuhakikisha usalama zaidi barabarani kwa lengo la kuokoa maisha. Katika kipindi kilichopita babu na mama yake Nelson walikuwa njiani kwenda kumtembelea hospitalini. Hata hivyo babu Peter alifanya pupa akataka kulipita lori bila kuona magari yaliyokuwa yakija mbele yao. Gari lake liligonga lori. Mamake Nelson alipatia fahamu hospitalini. Alikuwa na bahati sana kuwa hai kwani gari lenyewe liliharibika kwa kiasi kikubwa. Katika kipindi hiki, Alice, dada mdogo wa Nelson, anaelekea nyumbani kutoka shuleni akiwa pamoja na rafiki yake Nancy. Inawabidi kuvuka barabara kuu yenye magari mengi.

**Scene One: Walking home from school**

**2. SFX Atmo: children's voices leaving school, car noises in the background**

**3. NANCY:** (**walking along**) Hisabati naiona ngumu sana kwangu, Alice. Sielewi kabisa hiyo aljebra... Je una nafasi ya kunifunza? Wewe unaielewa zaidi yangu mimi... kwa muda wa saa chache tu?

**4. ALICE:** Kweli, Nancy. Mbona tusifanye sasa hivi? Mamangu bado angali hospitalini, na Nelson yuko pamoja naye kwa hivyo hakuna mtu mwengine nyumbani sasa hivi. Nishafanya karibu nusu ya kazi ya shule kwa hivyo tukirudi kwenu sasa tunaweza kupidia pamoja nusu ya kwanza. Lakini tunaweza kununua soda kwanza? Ninahisi kiu ajabu!

**5. NANCY:** Asante sana. Naam, tununue soda kwanza kwenye kioski pale kando ya barabara kuu. Kisha tutapanda basi upande wa pili wa barabara tuelekee nyumbani kwetu.

**6. ALICE:** Sawa hivyo.....

### **Scene Two: at kiosk**

**7. SFX Atmo: sound of cars going past on the busy highway**

**8. SFX: two bottles clinking**

**9. NANCY:** (**takes a nip from the bottle**) Vipi jamaa zako lakini?

**10. ALICE:** Hawana neno. Wazima hivyo hivyo hata baada ya ajali za siku mbili mfululizo. Baba hajamakinika tangu aliposababisha ajali, askari polisi wangali wakimhoji. Huenda atapokonywa kibali cha kuendesha magari. Hata sitaki kuyafikiria hayo.

**11. NANCY:** Lakini Nelson ni mzima? Na mamako je?

**12. ALICE:** Naam, sasa hana neno. Nadhani ana hofu kidogo tu. Tena akijua kwamba aliponea chupuchupu pale watu wawili walipofariki. Na mama – anachelea kupanda magari tena. Anakaa akisema jinsi alivyomtahadharisha babu kutoyapita magari wala hakufwata ushauri wake... sidhani kama atawahi kukubali kuendesha kwa gari na babu siku za usoni. Nina hakika ya hilo.

**13. NANCY:** Inshangaza jinsi watu wanavyoendesha magari hapa. Babako na babu yako kwa tajriba yao ya kuendesha gari kila siku kujipatia kipato, wanatakikana kuendesha magari yao kwa uangalifu. Lakini wanatenda kinyume..

**14. ALICE:** Ninajua. Jambo hilo limeitatiza familia yangu kidogo. Watu kulaumiana na wengine kuhisi vibaya.

**15. NANCY:** Acha nilipe soda, halafu tuondoke.

**16. SFX:** **sound of bottles clinking, coins on the counter**

**17. ALICE:** Naam, twende zetu. Ninachukia kuvuka barabara hii kila siku. Utadhani madereva huongeza magari kasi wanapokuona ukijiandaa kuvuka barabara. Madereva hawa utadhani ni vichaa!

**18. SFX:** **NOISE OF THE STREET COMES CLOSER**

**19. NANCY:** Hali si mbaya sana hivyo. Unatakikana kutazama kisha ukimbie kuvuka barabara. Nitatangulia... Tazama!

**20. ALICE:** Usiniambie unataka kuvuka sasa. Kuna gari linalokuja kwa kasi!

**21. NANCY:** **(shouting from the middle of the road)** Tayari nimefika katikati ya barabara! Utanipata upande wa pili...

**22. SFX:** **screeching of brakes, shouting**

**23. ALICE:** **(shouting)** Naaaannncyyyy, uko salama??? Mungu wangu??? **(runs to the middle of the road as cars slow down to see what has happened)**  
Unafanya nini, Nancy? Karibu upigwe dafrau!

**24. NANCY:** Nimeponea chupuchupu! Lau singepanda huu ukuta hali ingekuwa nyingine. Dereva mwenyewe amejitahidi kuliepsha gari kunigonga. Hata hivyo hajasimamisha gari lake, amejiondokea tu.

**25. ALICE:** Umenishtua sana. Mamangu yuko hospitalini, kakangu naye na ajali halafu wewe... Nancy tupande basi twende kwenu kabla ya kupatwa na makubwa tusiyoyaweza!

### **Scene Three: Nancy's house**

**26. SFX:** music in the background

**27. ALICE:** Sasa umeelewa angaa kidogo? Nadhani ni vyema upitie pitie mara kadha wa kadha na utafungukiwa. Nakwambia ukweli. Hivyo ndivyo aljebra ilivyo

**28. NANCY:** aaah labda. Nadhani inanibidi kuendelea kufanya mazoezi. Mtihani wetu ni lini, kiasi wiki mbili zijazo?

**29. ALICE:** Sidhani. Itakuwa mwisho wa juma lijalo. Ninapaswa kuondoka. Giza lishaingia. Mamangu hapendi niwe barabarani wakati kuna giza. Tutaonana kesho.

**30. NANCY:** Naam. Asante sana kwa msaada. Tutaona kesho!

**31. SFX:** door opening and closing

**Scene Four: On the road****32. SFX Atmo:** **road at night**

**33. ALICE:** **(walking along talking to herself)** Mbona hawana njia za watembea kwa miguu za kupita kando kando ya barabara? Ni hatari kutembea katikati ya barabara wakati wa usiku.

**34. SFX:** **bike bell ringing**

**35. CYCLIST:** **(screaming)** Tahadhari, sijakuona. Si vizuri kutembea gizani ukiwa na mavazi uliyovaa, hakuna...

**36. SFX:** **bike riding off**

**37. ALICE:** **(talking to self)** Naam, eti mimi nivae magwanda hayo yanayong'ara, si mimi wa kufanya hivyo... siwezi...

**38. SFX:** **sound of cars speeding up****39. SFX:** **Wing mirror hits person****40. ALICE:** **screaming****41. SFX:** **Car stops, door opens**

**42. DRIVER:** Je, uko salama? Sikukuona barabarani. Una bahati – nadhani kioo cha gari cha upande kimekupata begani. Uko sawa? Acha nikushikilie uinuke.

**43. ALICE:** (**Shouting**) Kwani akili yako ilikuwa wapi? Hata mwendo hujapunguza. Kwani hamjali watu wanaotembea barabarani? Hata kama mna magari haina maana kwamba barabara ni zenu peke yenu!

**44. DRIVER:** Taratibu, usinipigie kelele! Unataraji nikuone vipi? Umehaa fulana nyeusi na suruali ndefu nyeusi. Kwani una habari wewe? Unapotembea gizani unatakikana kuvali mavazi yanayong'ara ili madereva wakuone.

**45. ALICE:** Kwani hilo litabadilisha chochote? Nyinyi mnadhani kwamba ndio wenye haki ya kuwepo barabarani. Kupiga watu dafrau ovyo ovyo. Tazama unakokwenda.

**46. DRIVER:** Nisikilize msichana! Ningetaka ningejienda zangu na kukuacha ulipo lakini nimesimama kukusaidia. Lakini ukiendelea kunisemesha sitashughulika nawe. (**gets in car**)

**47. SFX:** door slamming, car driving off

**END OF SCENE FOUR**

**SHORT MUSIC**

**48. BEATRICE:** Naam, kama ulivyosikia katika kipindi cha tatu cha mchezo wetu wa redio kuhusu usalama barabarani, nusura mtu mwingine wa familia ya Wanjiru aangamie barabarani. Lakini je nini kilihitajika kufanyika kuzuia ajalai kama hiyo? Ninaye hapa studioni George, mtaalamu wa usalama barabarani ambaye atazungumzia jinsi ya kufanya marekebisho fulani madogo maishani mwetu ili tupate usalama barabarani. Karibu George!

**49. GEORGE:** Asante, Beatrice. Nadhani watembea kwa miguu na madereva wanapaswa kuheshimiana- heshima hiyo isipokuwepo ndipo unapokumbana na ajali kama hiyo ambayo tumeisikia.

**50. BEATRICE:** Ebu fafanua zaidi una maana gani unapozungumzia heshima ?

**51. GEORGE:** Mwanzoni mwa kipindi tunawasikia wasichana wakiwakashifu madereva kuwa hawawaheshimu watembea kwa miguu. Alice alisema madereva huwa kama kwamba wanaongeza kasi magari yao mtu anapotaka kuvuka. Madereva wanapaswa kuheshimu haki za watembea kwa miguu ambao ndio walio kwenye hatari barani Afrika kwani hawatengewa njia zao pembedi ya barabara.

**52. BEATRICE:** Kwa hivyo madereva wanapaswa kupunguza mwendo ili kuwapa nafasi watembea kwa miguu kuvuka barabara? Au pia kuendesha magari pole pole zaidi wanapowaona watu wakitembea kando kando ya barabara?

**53. GEORGE:** Naam. Bila shaka. Lakini pia watembea kwa miguu wanapaswa kuwaheshimu madereva wala wasiingie mahali ambapo madereva hao hawaona. Nancy alipovuka barabara yenyé magari mengi na kupanda ukuta, alianguka barabarani. Alikuwa na bahati sana kwa kuwa dereva alijitahidi kumwepuka. Alipaswa kuvuka barabara hiyo baada ya kuhakikisha kwamba hakuna gari lililokuwa likija.

**54. BEATRICE:** Wasemaje kuhusu Alice kutembea gizani alipokuwa akielekea nyumbani?

- 55. GEORGE:** Ilimbidi atembee barabarani. Hata hivyo alikuwa amevaa mavazi meusi. Vigumu sana kwa dereva kumuona kwa wakati ufaao. Lai angevaa mavazi yanayong'aa kama vile fulana nyeupe, hangekumbwa na yale yaliyomkumba. Kwa bahati nzuri hakuna aliyedhurika. Jambo la msingi tunalojifunza kwenye kipindi hicho ni kwamba ajali haziwapati abiria na madereva tu.
- 56. BEATRICE:** Na watembea kwa miguu nao wanatakikana kuchukua hatua gani?
- 57. GEORGE:** Unapotembea usiku, vaa nguo zinazong'ara. Kuwa mwangalifu unapovuka barabara- jipe muda wa kutosha kuivuka barabara- usihatarishe maisha yako. Unapojihatarisha jua kwamba unahatarisha pia maisha ya dereva anayehusika..
- 58. BEATRICE:** Asante sana George kwa kututembelea katika studio zetu.

**59. MUSIC (FADE UNDER OUTRO)**

**OUTRO**

**60. BEATRICE:** Katika kipindi kijacho tutasikia jinsi familia ya Wanjiri inavyoponea chupuchupu kwenye ajali nyingine kutoka na papara za madereva barabarani. Kama unataka kusikiliza kipindi kwa mara nyingine, tazama wavuti wetu [www.dw.de/lbe](http://www.dw.de/lbe). Tunakushukuru kwa kujunga nasi na hakikisha kwamba kuna usalama barabarani!